

KUHUSU SISI

- Karibu SKMIHAS kujenga kesho yako unayoitegemea.
- SKMIHAS ni Taasisi binafsi, inayomilikiwa na Dayosisi ya Morogoro, pia chuo kimesajiliwa na NACTVET kwa namba ya Usajili REG/HAS/260.
- Chuo kipo Mikumi, kilometa sita (6) kutoka hifadhi ya Taifa ya Mikumi. Chuo kina mazingira yenye uoto mzuri wa asili pamoja na majengo yenye huduma za kisasa.
- CHUO kinafikika kwa urahisi sana, karibu na barabara kuu ya Dar es Salaam -Mbeya.
- Chuo kina walimu wenye uzoefu na ufanisi, ambao watawaongoza wanafunzi kwenye Ngazi ya stashahada ya Uuguzi na Ukunga (inayoanza 2024) pamoja na stashahada ya Huduma ya Mazoezi Tiba (inayoanza 2025).
- Chuo kipo eneo moja na Hospitali ya Mkatifu Kizito Mikumi. Hospitali yenye viwango vya hali ya juu pamoja na kukidhi mahitaji ya kusoma kwa ajili ya Chuo.
- Chuo kina sehemu salama za malazi, hosteli nzuri sana kwa ajili ya wasichana. Pia chuo kinatoa huduma ya chakula.
- Ada na gharama nyingine zinaweza kulipwa kwa awamu, kwa mwezi au kila muhula.
- Tunapenda kuwakaribisha wanafunzi wote na tutawahudumia kwa misingi yote.



SKMIHAS KWA TAARIFA ZAIDI:



+255-763-167-831

+255-657-077-152



skmihhas01@gmail.com



MAHALI: Mikumi



TOVUTI: www.skmihhas.ac.tz



Saint Kizito Mikumi Institute of Health and Allied Sciences



KWA NINI MTUCHAGUE SISI

- Viwango vya hali ya juu katika elimu ya afya na ufundishaji.
- Chuo kitafata mtaala mpya wa taifa katika ufundishaji
- Chuo kinatumia vifaa vipya na vya kisasa pamoja na sanamu ya binadamu katika kujifunza.
- Chuo kina vyumba vikubwa vyenye nafasi pamoja na madarasa yenye kompyuta nyingi kwa ajili ya wanafunzi kujisomea binafsi.
- maktaba ya kisasa iliyosheheni vifaa madhubuti ikiwemo vitabu vya kielektroniki kwa ajili ya kusoma.
- Vyumba vikubwa vyenye nafasi na vifaa vyote muhimu kwa ajili ya mitihani na mikutano, pamoja na fenicha bora za kisasa kwa Masomo.
- Mbao kubwa za Matangazo, Runinga na projekta, zinatumiwa na Chuo katika ufundishaji.
- Chuo kina vifaa vingi vya kisasa kwa ajili ya manesi kujifunzia na kufanyia mazoezi.
- Hosteli kubwa zenye hadhi, na vyumba vizuri vyenye vyoo na mabafu ya kisasa.
- Chuo kipo eneo moja na Hospitali ya Mt.Kizito; hivyo kufanya masomo ya vitendo kuwa rahisi.
- Chuo kinazungukwa na Mazingira safi, yenye uoto wa asili, unaofanya mazingira ya kujisomea binafsi, au makundi yawe rafiki sana.



MAONO

Kuwa muhimili wa ufanisi ambao utafikiwa na kila mwanafunzi mwenye vigezo stahiki.
Kutoa elimu bora, ili kila mwanafunzi atimize lengo.
Dhumuni lengo letu pia ni kukuza na kuboresha huduma za afya Tanzania hususani, lakini pia Afrika kwa ujumla.



ELIMU ZITOLEWAZO

Uuguzi na Ukunga

Elimu hii inalengo la kuelimisha wauguzi na wakunga kutatua mahitaji ya kiafya ya muda mfupi, na baadae kwa Watanzania.



Elimu ya Mazoezi Tiba

Wahitimu wa elimu hii wanalenga kutoa huduma za mazoezi tiba kwa ufanishi mkubwa sana kitaaluma.

